

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 2



## 76 Hezekia anaamini kwa Mungu

### Kwa Biblia

2 Wafalme mlango wa 18:28 – 37 na mlango wa 19:1 – 16, 32 – 37

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu ako karibu na wote wampendao. Hakuna kisicho wezekana tukiwa na imani kwa Mungu

### Somo

Watu wa Mungu waliishi kwa falme mbili. Ufalme wa kaskazini uliitwa Israeli na ulikuwa na makabili kumi. Ufalme wa kusini uliitwa Yuda na ulikuwa na makabila mawili.

Kwa miaka mingi, watu wa ufalme wa kaskazini waliasi amri za Mungu. Waliabudu sanamu za mbao na mawe. Hawakupenda Mungu lakini bado Mungu alipenda taifa la Israeli. Alitaka watu wamrudie. Mungu aliongoja taifa la Israeli kwa miaka 200 ili watubu na wamrudie. Lakini hawakutubu. Bado waliabudu sanamu.

Ashuru lilikuwa taifa kubwa. Waashuru walipigana na Waisraeli. Walichukua sehemu moja ya Israeli. Kila mwaka Mfalme Waashuru alifanya watu wa Israeli walipe pesa nyingi sana kama kodi. Mwaka moja watu wa Israeli walikataa. Walikataa kulipa kodi kwa Mfalme wa Ashuru.

Mfalme wa Ashuru alikasirika sana. Aliongoza jeshi lake kupigana na Waisraeli. Waashuru walizingira Samaria mji mkuu wa Israeli.

### Maswali


1. Taifa la Israeli lilipenda na kumtii Mungu?
2. Taifa gani kubwa lilikuja kushambulia Israeli?
3. Watu wa Israeli waliamini Mungu?
4. Nini ilifanyika kwa watu wa Israeli?
5. Mfalme wa Ashuru alitumia Hezekia Mfalme wa Yuda ujumbe eti nini?
6. Hezekia alifanya nini?
7. Mfalme wa Ashuru alitumia Hezekia nini?
8. Hezekia alifanyaje hiyo barua?
9. Mungu alitumia Hezekia ujumbe gani?
10. Nini ilifanyika kwa Waashuru?

### Majibu

1. La. Watu wa Israeli waliabudu sanamu.
2. Waashuru walishambulia Israeli.
3. La.
4. Walichukuliwa mateka baada ya kuzingirwa kwa muda mrefu.
5. Usimwamini Mungu. Hatakuokoa kutoka kwa Waashuru.
6. Hezekia aliomba Mungu. Alitumanisha wamuite nabii Isaya.
7. Alitumia barua akisema kwamba Mungu hatamwoko.
8. Hezekia alipeleka barua kwa nyumba ya Mungu na akaomba.
9. “Usiogope. Waashuru hawatashambulia Yerusalemu.”
10. Tauni iliua Waashuru 185,000. Walirudi nyumbani. Mfalme wao aliuawa.

Mfalme wa Ashuru na jeshi lake walizingira Samaria. Hakukuwa na mtu wa kutoka wala kuingia mjini. Walizingira huo mji kwa miaka mitatu. Baada ya miaka mitatu, watu wa Samaria hawakuwa na chakula. Walijisalamisha kwa Waashuru. Mfalme wa Ashuru alichukua watu wa Israeli wote waende kuishi Ashuru kama watumwa.

Mfalme Hezekia wa Yuda naye alikataa kulipa Waashuru kodi kwa mwaka mmoja. Jeshi la Ashuru lilienda kupigana na Yuda. Waashuru waliharibu vijiji vingi. Jeshi lilienda na likashambulia Yerusalemu, mji mkuu wa Yuda.



Mfalme wa Ashuru alituma wajumbe kwa Hezekia mfalme wa Yerusalemu. Wajumbe wa Ashuru walisema huo ujumbe kwa sauti ili watu wa Yerusalemu wasikie. Watu wa Yerusalemu walikusanyika kwa ukuta wa Yersalemu. Walisikiliza ujumbe kutoka kwa Mfalme wa Ashuru. Waashuru walijaribu kutetemesha kila mtu.

Wajumbe wa Ashuru walipasa sauti wakisema, “Msimkilize Hezekia. Hawezi kumwokoa kutoka kwa Waashuru. Hezekia atamwambia mwamini kwa Mungu. Msimkilize. Mungu wenu hatawaokoa kutoka kwa jeshi kuu la Ashuru. Tumeshinda nchi nyingi. Miungu ya zile nchi hasikuokoa watu wake. Mungu wenu hawezi kumwokoa kutoka kwa Waashuru. Jisalimishe kwa Mfalme wa Ashuru.

Watu wa Yerusalemu walikuwa wamehadharishwa kwamba wasizungumze na wale wajumbe. Walisikiliza ujumbe wakiwa kimya. Mfalme Hezekia alisikia ujumbe. Kuonyesha kwamba amesikitika, alirarua nguo zake na kujipaka majivu kichwani mwake. Hezekia aliomba Mungu. Aliomba Mungu awasaidie.

Hezekia alitumanisha wamuite nabii Isaya. Isaya aliletea Hezekia ujumbe kutoka kwa Mungu. Mungu alisema, “Msiwaogope Waashuru. Nitawafanya warudi kwa nchi yao. Mfalme wa Ashuru atarudi kwa nchi yake na atakufia kule.”

Mfalme wa Ashuru alitumia Hezekia barua. Alisema hivi, “Mungu wako hawezi kukuokoa. Mungu wako hatazuia Waashuru kupiga na kuchukua Yerusalemu. Tumepiga na kuharibu nchi nyingi. Tutakuja na kuharibu Yerusalemu na Yuda. Hakuna miungu wa nchi zingine wenye wamewahi kuokoa watu wake. Mungu wako hataweza kukuokoa.”

Hezekia alichukua hiyo barua na akaipeleka kwa nyumba ya Mungu. Aliomba Mungu, “Ee Bwana Mungu, Wewe ni Mungu wa falme zote duniani. Wewe ni Mungu Mkuu uliyeziumba mbingu na nchi. Tafadhali tuokoe kutoka kwa Waashuru. Tafadhali onyesha Nguvu na uwezo Wako ili mataifa yote yajua kwamba Wewe ni Bwana Mungu. Wewe ndiwe Mungu wa pekee.”

Hezekia aliamini Mungu na Mungu akamwokoa kutoka kwa Waashuru. Isaya alileta ujumbe mwingine kutoka kwa Mungu. Mungu alimwambia Hezekia, “ Mfalme Waashuru hatakuja kwa huu mji. Tena hatatupa mshale. Atarudi kwa nchi yake.”

Waashuru walikuja kushambulia Yerusalemu. Walikuja mpaka kijiji cha Nobu kilicho karibu na Yerusalemu. Waashuru walipiga kambi Nobu. Usiku huo Mungu alituma tauni. Kwa jeshi la Waashuru watu 185,000 waliuawa kwa tauni. Waashuru walitishika sana. Kulipokucha, Waashuru walitoroka. Walirudi Ashuru kwa nchi yao. Mfalme wa Ashuru aliporudi nyumbani aliuawa na wanawe wawili.

Hili somo linatufundisha kwamba Mungu ako karibu na wote wanaompenda. Hakuna lisilowezezana kwa Mungu. Hakuna nguvu inayoweza kushinda Mungu. Taifa la Israeli halikusikiliza Mungu. Walichukuliwa mateka na Waashuru. Hezekia na taifa la Yuda waliamini Mungu. Mungu aliwaokoa kutoka kwa jeshi kuu la Waashuru.

